# BIBLIA YASEMA NINI KUHUSU MARIAMU?

### JE! MARIAMU ASTAHILI SIFA?

Bila shaka Mariamu alikuwa mtu mwema na asingalichaguliwa na Mungu kumpata mtoto kama angalikuwa mwovu. Mariamu mwenyewe alimtukuza Mungu akisema, "Na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu; kwa kuwa ameutazama unyonge wa mjakazi wake. Kwa maana, tazama, tokea sasa vizazi vyote wataniita mbarikiwa." Lk. 1:47-48.

### MARIAMU ATUKUZWE KULIKO WENGINE?

Mpaka leo wanadamu humwita Maraiamu kuwa mbarikiwa. Walakini, baraka ambayo alipata Mariamu ni ile ile ya kumzaa na kumlea Yesu. Hebu! Tusikie maneno ya mwenyewe, "Akaletewa habari akaambiwa, Mama yako na ndugu zako wamesimama nje wakitaka kuonana nawe. Akawajibu akasema, Mama yangu na ndugu zangu ndio hao walisikiao neno la Mungu na kulifanya," Lk. 8:20-21.

Hapo Yesu amesema waziwazi kwamba mama hakustahili sifa kuliko mtu ye yote afanyaye mapenzi ya Mungu.

### JE! TUOMBE KWA MARIAMU?

Baadhi ya watu husema kwamba inafaa kuomba kwa Mariamu kwa sababu yeye akiwa mwanamke, ataweza kutuonyesha huruma na upendo wa kimama. Je! Mariamu aliyeumbwa na Mungu alikuwa na upendo na huruma kuliko Mungu mwenyewe? La! Hasha! Bali Mariamu alifundishwa upendo na Mungu. Twasoma 1 Yoh. 4:16, 19, "Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake....Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza."

Hakuna hata mstari moja katika Biblia unaoturuhusu kuomba kwa Mariamu. La! Bali twasoma:

"Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu." 1 Tim. 2:5.

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chine ya mbingu waliloewa wanadamu litupasalo sis kuokolewa kwalo." Mdo. 4:12.

"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye." Kol. 3:17.

“Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana.” Yoh. 14:13.

Mstari hii yasema waziwazi kwamba Mariamu siye mpatanishi wetu. Tena, yatuamuru kufanya kila tendo na kila neno kwa jina la Yesu ambalo ni jina pekee tulilopewa liletalo wokovu.

**JE! MARIAMU NI MAMA WA MUNGU?**

Yesu alisema kwamba Mungu ni roho (Yoh. 4:24) na kwamba roho haina mwili na mifupa (Lk. 24:39). Tena, Yesu alisema: “Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho” (Yoh. 3:6). Kwa hiyo, ni waziwazi kwamba Mariamu (aliye mwili) hakumzaa Mungu (aliye roho). Mariamu alizaa mwili wa udongo Yesu bali roho wa Yesu alitoka kwa Mungu mwenyewe!

Watu wengi hufikiri kwamba Yesu hakuwapo kabla ya Mariamu kuzaa mtoto. Biblia huonyesha kwamba Yesu alikuwapo kwa Mungu (katika hali ya roho) kabla Mungu hajaumba kitu. Wala haitoshi, bali kila kitu kilichoumbwa na Mungu kiliumbwa kwa njia ya Yesu. Twasoma:

“Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana: ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikamana katika yeye.” Kol. 1:16-17.

“Hapo mwanzo kulikuwa Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika....alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua....Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.” Yoh. 1:1-3, 10, 14.

Katika mistari hii, twaona kwamba Yesu alikuwapo kabla ya vitu vyote tena kwamba vitu vyote viliumbwa na yeye. Kwa hiyo, Mariamu mwenyewe aliumbwa na Yesu! Basi, Mariamu amewezaje kuitwa mama yake yule aliyemwumba?

Jibu ni kwamba Mariamu alikuwa mama wa mwili ya Yesu wala si wa Roho wake. Basi, kwa sababu Mungu ni Roho, Mariamu hawezi kuitwa mama wa Mungu (Yoh. 4:24; Lk. 24:39).

**JE! MARIAMU ALIZAA WATOTO WANGAPI?**

Kuzaa mtoto si dhambi!  Mungu mwenyewe ametuumba na uwezo huu!  basi, mbona watu hufikiri kwamba ingekuwa dhambi kwa Mariamu na Yusufu kama wangalizaa watoto?  tusome Biblia:

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.  Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi."  Mwa. 1:27-28.

"Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu."  Ebr. 13:4.

"Tazama, wana ndio urithi wa Bwana, uzao wa tumbo ni thawabu."  Zab. 127:3.

Kuzaa mtoto siyo dhambi.  La!  bali ikiwa Mariamu angalimnyima Yusufu bwana wake haki yake ya mume, basi hapo kweli Mariamu angalikuwa mwenye dhambi, maana twasoma:

"Mume na ampe mkewe haki yake, na vivyo hivyo mke na ampe mumewe haki yake.  Mke hana amri juu ya mwili wake, bali mumewe;  vivyo hivyo mume hana amri juu ya mwili wake, bali mkewe.  Msinyimane isipokuwa mmepatana kwa muda, ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, Shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu."  1 Kor. 7:3-5.

Biblia yaonyesha kwamba Mariamu alizaa watoto wengine baada ya Yesu.

"Alipokuwa katika kusema na makutano, tazama, mama yake na ndugu zake walikuwa wakisimama nje, wataka kusema naye.  Mtu mmoja akamwambia, Tazama, mama yako na ndugu zako wamesimama nje, wanataka kusema nawe.  Akajibu, akamwambia yule aliyempasha habari, Mama yangu ni nani?  Na ndugu zangu ni akina nani?  Akawanyoshea mkono wanafunzi wake, akasema, Tazama, Mama yangu na ndugu zangu!  Kwa maana ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu."  Mat. 12:46-50.

Katika mistari hii, watu wale waliompasha Yesu habari walitaka kuwaheshimu mama na ndugu wa Yesu wa kimwili.  Yesu aliwafundisha kwamba mwanafunzi ye yote afanyaye mapenzi ya Mungu ni ndugu wa kiroho mwenye thamani kwake sawa sawa na mama na ndugu zake wa kimwili.

"Na alipofika nchi yake, akawafundisha katika sinagogi lao, hata wakashangaa, wakasema, Huyu amepata wapi hekima hii na miujiza hii?  Huyu si mwana wa seremala?  Mamaye si yeye aitwaye Mariamu?  Na nduguze si Yakobo, na Yusufu, na Simoni, na Yuda?  Na maumbu ya ke wote hawapo hapa petu?  Basi huyu amepata wapi haya yote?  Wakachukizwa naye.  Yesu akawaambia, Nabii hakosi kupata heshima, isipokuwa katika nchi yake, na nyumbani mwake mwenyewe."  Mat. 13:54-57.

Mistari hii yasema kwamba Yesu alifika nchi yake na nyumbani mwake mwenyewe. Kwa hiyo, watu wote walimtambua kuwa mwana wa Mariamu na kaka wa Yakobo, Yusufu, Simoni na Yuda na maumbu (Dada) zake waliokuwapo wote pale pale! Mwanzoni, hata wadogo hawa wa Yesu mwenyewe hawakumwamini. Twasoma: "Na sikukuu ya Wayahudi, Sikukuu ya vibanda, ilikuwa karibu. Basi ndugu zake wakamwambia, ondoka hapa, uende Uyahudi, wanafunzi wako nao wapate kuzitazama kazi zako unazozifanya. Kwa maana hakuna mtu afanyaye neno kwa siri, naye mwenyewe ataka kujulikana. Ukifanya mambo haya, basi jidhihirishe kwa ulimwengu. Maana hata nduguze hawakumwamini." Yoh. 7:2-5.

Baada ya Yesu kufufuka katika wafu, wadogo zake nao walikuwa wakimwamini. Twasoma:

"Hata walipoingia, wakapanda orofani, walipokuwa wakikaa; Petro, na Yohana, na Yakobo, na Andrea, Filipo na Tomaso, Bartholomayo na Mathayo, Yakobo wa alfayo, na Simoni Zelote, na Yuda ya Yakobo. Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali, pamoja nao wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake." Mdo. 1:13-14.

Basi, baada ya kufufuka kwake Yesu twasoma habari ya Yakobo, ndugu yake Bwana, mara nyingi katika Biblia. Yakobo huyo daima huitwa "ndugu wa Bwana" kusudi tuweze kupambanua kati yake yey na Yakobo yule mwingine aliyekuwa mtume. Yakobo, ndugu wa Bwana, alisifiwa kuwa nguzo katika kanisa la Yerusalmu. Mtume alisema:

"Kisha, baada ya miaka mitatu, nalipanda kwenda Yerusalemu ili nionane na Kefa, nikakaa kwake siku kumi na tano. Lakini sikumwona mtume mwingine, ila Yakobo, ndugu yake Bwana.... Kisha, baada ya miaka kumi na minne, nalipanda tena kwenda Yerusalemu pamoja na Barnaba, nikamchukua na Tito pamoja nami.....Yakobo, na Kefa, na Yohana, wenye sifa kuwa ni nguzo, walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika; ili sisi tuende kwa Mataifa, na wao waende kwa watu wa tohara." Ga. 1:18-19; 2:1, 9.

Wadogo hawa wa Yesu walioa sawa sawa na Petro (Kefa) na mitume wengine.

"Hatuna uwezo kushukua pamoja nasi mke aliye ndugu, kama wao mitume wengine, na ndugu wa Bwana, na Kefa?" 1 Kor. 9:5.

Bila shaka mistari hii yatosha kumwonyesha mwenye kupenda kweli kwamba Mariamu alizaa watoto wengine baada ya kumzaa Yesu. Yesu alizaliwa bila baba wa kimwili, bali Yusufu alikuwa baba wa watoto hawa wengine. Hata hivyo, kwa sababu Yesu na watoto hawa wengine walikuwa na mama moja (Mariamu), walikuwa ndugu zake Yesu.